


SHERIA ZA KIPEKEKEE KWA ULINZI WA AINA ZA MIMEA NA HAKI ZA WAZALISHAJI WA MIMEA

Shirika la Biashara Duniani (WTO), ambalo linashughulika na sheria za biashara kati ya mataifa wanachama, lina makubaliano yanayofahamika kama 'vipengele Vinavyohusiana na Biashara ya Hakimiliki za Kazi za Kitaaluma (TRIPs). Nchi 42 za Afrika ni wanachama wa Shirika la Biashara Duniani na makubaliano ya Hakimiliki za Kazi za Kitaaluma (TRIPs).

Masharti ya Makubaliano ya TRIPs yanawataka wanachama wa Shirika la WTO kutoa ulinzi wa aina za mimea kupitia haki za wazalishaji wa mimea. Huruhusu nchi kuweka mfumo wowote wa Haki za Wazalishaji wa Mimea ambao utatosheleza mahitaji ya mifumo yao ya kilimo na hali ya uchumi. Huu ni mfumo unaojulikana kama '*sui generis*' (mfumo wa kipekee).

NCHI ZILIZO NYUMA KIMAENDELEO

Nchi nyingi za Afrika zina uzoefu mdogo sana au hazina kabisa na Haki za Wazalishaji wa Mimea, au na sekta binafsi ya mbegu. Lakini, ijapokuwa Nchi Zilizyo Nyuma Kimaendeleo hazilazimiki kuweka mfumo wowote wa Ulinzi wa Aina za Mimea hadi Julai 2021 – na wanaweza kuongezewa muda baada ya hapo– Nchi nyingi Zilizyo Nyuma Kimaendeleo katika bara la Afrika zinakimbilia kupitisha mifumo ya taifa na kanda ya Haki za Wazalishaji wa Mimea inayotokana na Muungano wa Kimataifa wa Kulinda Aina za Mimea (UPOV) wa mwaka 1991, makubaliano ya kimataifa ambayo yanapendelea uzalishaji wa mbegu za kibiashara.



Nchi zinazoendelea kama vile Malaysia, India na Thailand wana mifumo ya kipekee ya Haki za Wazalishaji wa Mimea. Mifumo hii hulinda haki za wakulima. Ni muhimu kwa wadau wote kuhusika katika kutayarisha mfumo wa kipekee wa Haki za Wazalishaji wa Mimea kwa nchi nzima ili kusawazisha maslahi ya makundi yote yanayohusika, wakiwemo wakulima, walaji, jamii za wenyeji na wazalishaji wa mbegu. Mfumo huu wa kipekee usikinazane na mfumo wa mbegu unaosimamiwa na mkulima au kujaribu kuubadilisha na mfumo mwingine, kama ambavyo Muungano wa Kimataifa wa Kulinda Aina za Mimea (UPOV) unavyofanya.

